JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# UTAFITI WA WATU WENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI 2020/21

## VIASHIRIA MUHIMU VYA SOKO LA AJIRA

Septemba 2021

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| 1.0 Ajira kwa Sekta Kuu za Kiuchumi (Employment by Main Industry) | 4 |
| 2.0 Hali Katika Ajira (Status in Employment) | 5 |
| 3.0 Ajira kwa Sekta (Employment by Sector) | 7 |
| 4.0 Ajira kwa Aina ya Kazi (Employment by Occupation) | 9 |
| 5.0 Ushiriki Katika Shughuli za Kiuchumi kwa Watu Wenye Ulemavu (Participation of Disabled Persons in Economic Activities) | 11 |
| 6.0 Kiwango cha Ushiriki Katika Nguvu Kazi (Labour Force Participation Rate) | 12 |
| 7.0 Uwiano wa Ajira kwa Idadi ya Watu Wenye Umri wa Miaka 15 + (Employment to Population Ratio) | 13 |
| 8.0 Saa za Kazi (Hours of Work) | 15 |
| 9.0 Ajira Katika Sekta Isiyo Rasmi (Informal Sector) | 18 |
| 10.0. Kiwango cha Ukosefu wa Ajira (Unemployment Rate) | 20 |
| 11.0 Ukosefu wa Ajira kwa Vijana | 22 |
| 12.0 Ukosefu wa Ajira wa Muda Mrefu (Long Term Unemployment) | 25 |
| 13.0 Ajira Zisizotimilifu (Underemployment) | 26 |
| 14.0 Kiwango cha Watu Walio Nje ya Nguvu Kazi (Inactivity Rate) | 27 |
| 15.0 Elimu na Kutojua Kusoma na Kuandika (Education Attainment and Illiteracy) | 28 |
| 16.0: Wastani wa Mshahara na Ujira (Average Direct Wages and Salaries) | 30 |


Hakimiliki © 2021 – NBS na OCGS

# DIBAJI

Taarifa hii inawasilisha matokeo Muhimu ya Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi (ILFS) uliofanyika Tanzania Bara na Zanzibar kuanzia mwezi Julai 2020 hadi mwezi Juni 2021. Utafiti huu ulifanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (OCGS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Rais-Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Utafiti wa mwaka 2020/21 ni wa sita kati ya tafiti zilizofanywa na Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo na wadau wengine.

Historia ya Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi kwa Tanzania Bara ulianza tangu mwaka 1965 ukiwa ni utafiti wa kwanza kufanyika baada ya uhuru. Utafiti huu ulifuatiwa na tafiti nyingine zilizofanyika mwaka 1990/91, 2000/2001, 2006 na 2014. Lengo la tafiti hizi ilikuwa ni kukusanya viashiria muhimu vya soko la ajira na takwimu nyingine za kijamii na kiuchumi ambazo zinazohitajika katika uundaji wa sera za kukuza ajira na ufuatiliaji wa mienendo ya ajira na ukosefu wa ajira kama inavyobainishwa kwenye dhamira mbalimbali za maendeleo kitaifa, kikanda na kimataifa zikiwemo:- Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano; Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2025; Dira ya Maendeleo ya Zanzibar, 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Dira ya Maendeleo ya Afrika ya Mashariki 2050; na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia ya 2030 ambayo yamejikita kwenye ukuaji endelevu wa uchumi na kazi zenye staha.

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Umoja wa Ulaya (EU) kwa kutoa msaada wa fedha kwenye Utafiti huu. Vile vile nashukuru makundi mbalimbali ya washiriki kwa juhudi zao zilizochangia katika uandaaji wa ripoti hii. Shukrani za pekee ni kwa Washirika wa Maendeleo hususan Benki ya Dunia (WB), Ofisi ya Nje, Jumuiya ya Madola na Maendeleo – FCDO na Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kutoa msaada wa kiufundi.

Shukrani za pekee ziende kwa timu tendaji ya Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2020/21 ya NBS na OCGS kwa usimamizi wao wa karibu katika hatua zote za utekelezaji wa utafiti ikiwa ni pamoja na; utayarishaji wa zana za utafiti, ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi na uandishi wa ripoti. Pia nathamini ushiriki wa dhati wa timu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu na Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa uwajibikaji ambao ulisaidia kufanikisha kukamilika kwa utafiti na ripoti hii.

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru wahojiwa wote hasa wazazi, watoto na wananchi wote kwa ujumla ambao walikubali kutenga muda wao kwa ajili ya mahojiano na kutoa taarifa muhimu ambazo zimewezesha NBS na OCGS kupata taarifa zinazohitajika.

**Dkt. Albina Chuwa**
Mtakwimu Mkuu wa Serikali
Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Mayasa M. Mwinyi**
Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ofisi ya
Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar

Hakimiliki © 2021 – NBS na OCGS

# UTANGULIZI

Kitabu hiki kinawasilisha matokeo ya Viashiria Muhimu vya Soko la Ajira kutoka katika Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi (ILFS), wa mwaka 2020/21. Viashiria hivi vimetolewa kwa ngazi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT); Tanzania Bara (TZB); na Zanzibar (ZNZ). Viashiria Muhimu vya Soko la Ajira ni nyenzo ya kimkakati kwenye uundaji wa sera za kukuza ajira na ufuatiliaji wa mienendo ya ajira na ukosefu wa ajira kama inavyobainishwa kwenye dhamira mbalimbali za maendeleo kitaifa na kimataifa zikiwemo:- Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano; Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2025; Dira ya Maendeleo ya Zanzibar, 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Dira ya Maendeleo ya Afrika ya Mashariki 2050; na Mpango wa Maendeleo Endelevu, 2030 (SDG). Dira hizi kwa ujumla zinasisitiza kupunguza Viwango vya Ukosefu wa Ajira; kuongeza vipato na kupunguza umaskini. Kitabu hiki kinaonesha matokeo ya Viashiria vya Soko la Ajira kwa watu wenye umri wa miaka 15 au zaidi, na maelezo yametolewa kwa kuzingatia tafsiri za kitaifa za viashiria hivyo.

Dhana na tafsiri za Viashiria vya Soko la Ajira zilizotumika katika Kitabu hiki zinatokana na mapendekezo ya kimataifa, hususan Mkutano wa Kimataifa wa Watakwimu wa Masuala ya Kazi wa Mwaka 1982. Hata hivyo, baadhi ya tafsiri hizo, hasa tafsiri ya ajira na ukosefu wa ajira, zimeboreshwa ili ziakisi hali halisi ya nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania. Tafsiri ya ajira kimataifa, inahusisha watu wote waliofanya shughuli ya kiuchumi angalau kwa saa moja kwenye kipindi cha rejea cha utafiti. Tafsiri ya ajira kitaifa ni sawa na ya kimataifa isipokuwa inaondoa watu wenye kazi hafifu (marginally attached to employment) kwenye kundi la wenye ajira na kuwajumuisha kwenye kundi la wenye ukosefu wa ajira.

[1] Watu wenye kazi hafifu (marginally attached to employment) kwa mujibu wa tafsiri ya taifa ya ukosefu wa ajira inajumuisha wasaidizi wanaofanya kazi bila malipo kwenye shughuli za kilimo; na pia wale wanaofanya kazi zisizo za kilimo bila uhakika wa kuwa na kazi hizo kwa kipindi cha mwezi unaofuata baada ya mwezi wa utafiti. Aidha, watu hao pia walifanya kazi hizo chini ya saa 40 kwa wiki; na walitaja sababu za kiuchumi kama kikwazo cha kutofanya kazi zaidi.

Hakimiliki © 2021 – NBS na OCGS

# 1.0 AJIRA KWA SEKTA KUU ZA KIUCHUMI (EMPLOYMENT BY MAIN INDUSTRY)

Ajira kwa sekta kuu za kiuchumi kinaonesha mgawanyo wa watu wanaojishughulisha na shughuli za kiuchumi katika sekta kuu za kichumi. Mgawanyo huu wa ajira kisekta unaonesha ukuaji wa uchumi unategemea sekta zipi za kichumi. Na taarifa za kiashiria hiki zinasaidia kupanga sera, programu na mikakati mbalimbali ya ukuzaji ajira na uchumi nchini.

**Jedwali 1.1: Asilimia ya Idadi ya Ajira kwa Sekta Kuu za Kiuchumi, Wenye Miaka 15+ (Tafsiri ya Kitaifa)**

| Sekta Kuu za kiuchumi | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 63.2 | 69.4 | 66.2 | 63.9 | 69.9 | 66.9 | 38.3 | 44.0 | 40.8 | 61.8 | 60.4 | 61.1 | 62.6 | 60.9 | 61.8 | 36.8 | 33.8 | 35.5 |
| Viwanda | 9.8 | 3.4 | 6.7 | 9.6 | 3.2 | 6.5 | 14.7 | 14.5 | 14.6 | 11.3 | 4.5 | 8.0 | 11.1 | 4.3 | 7.8 | 18.6 | 15.0 | 17.1 |
| Huduma | 27.0 | 27.2 | 27.1 | 26.4 | 26.9 | 26.7 | 47.0 | 41.6 | 44.6 | 26.8 | 35.2 | 30.9 | 26.3 | 34.8 | 30.5 | 44.6 | 51.3 | 47.4 |
| **JML** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Jedwali 1.2: Asilimia ya Idadi ya Ajira kwa Sekta Kuu za Kiuchumi, Wenye Miaka 15 + (Tafsiri ya Kimataifa)**

| Sekta Kuu za Kiuchumi | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 64.6 | 70.3 | 67.4 | 65.3 | 70.8 | 68.1 | 38.1 | 43.8 | 40.6 | 61.8 | 60.4 | 61.1 | 62.6 | 60.9 | 61.8 | 36.8 | 33.8 | 35.5 |
| Viwanda | 9.5 | 3.4 | 6.5 | 9.3 | 3.1 | 6.3 | 15.2 | 14.6 | 14.9 | 11.3 | 4.5 | 8.0 | 11.1 | 4.3 | 7.8 | 18.6 | 15.0 | 17.1 |
| Huduma | 25.9 | 26.4 | 26.2 | 25.4 | 26.0 | 25.7 | 46.8 | 41.6 | 44.5 | 26.8 | 35.2 | 30.9 | 26.3 | 34.8 | 30.5 | 44.6 | 51.3 | 47.4 |
| **JML** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Ujumbe muhimu: Jedwali 1.1** linaonesha uelekeo wa ajira nchini, ambapo mchango wa ajira katika kilimo, misitu na uvuvi kwa kutumia tafsiri ya Kitaifa umepungua kutoka asilimia 66.2 mwaka 2014 hadi asilimia 61.1 mwaka 2020/21, wakati sekta ya viwanda imeongezeka kutoka asilimia 6.7 mwaka 2014 hadi asilimia 8.0 mwaka 2020/21 na ajira katika sekta ya huduma imeongezeka kutoka asilimia 27.1 mwaka 2014 hadi asilimia 30.9 mwaka 2020/21.

Mahuasiano ya Kisera: Kupungua kwa idadi ya watu wanaoajiriwa katika sekta ya kilimo na kuongezeka ajira katika sekta ya viwanda na huduma kunaashiria mapinduzi makubwa ya kiuchumi jambo ambalo ni dalili njema ya maendeleo ya kiuchumi. Idadi ya waajiriwa katika sekta ya kilimo inapopungua na kuongezeka ajira katika sekta nyingine hususan viwandani na huduma inatoa ujumbe kwamba sekta ya kilimo inahudumiwa na watu wachache zaidi na hivyo tija huenda imeongezeka. Vilevile, mabadiliko haya yanaonesha kwamba ajenda ya vTanzania ya viwanda inazaa matunda na wakati huo huo ujuzi wa watu wetu uonaongezeka na kuweza kuajirika katika sekta ya viwanda na huduma ambazo kwa kawaida zinahitaji watu wenye ujuzi zaidi.

Hakimiliki © 2021 – NBS na OCGS

# 2.0 HALI KATIKA AJIRA (STATUS IN EMPLOYMENT)

Kiashiria cha Hali katika Ajira kinalinganisha aina sita za hali za ajira, yaani:- wafanyakazi wa kulipwa; wafanyakazi waliojiajiri (sio kwenye kilimo); wasaidizi wa kazi za familia za kiuchumi ambao pia wanajulikana kama wafanyakazi wa familia wasiolipwa na wafanyakazi wengine nje ya makundi hayo (Wanagenzi, Walio kwenye mafunzo ya Vitendo n.k). Kiashiria hiki kinaonesha mgawanyo wa ajira katika makundi sita ya ajira yaliyoainishwa.

**Jedwali Na. 2.1: Asilimia ya Watu Walioajiriwa kwa Hali za Ajira, Wenye Miaka 15+ (Tafsiri ya Kitaifa)**

| Hali ya Ajira | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Wafanyakazi wanaolipwa | 18.4 | 9.8 | 14.1 | 17.9 | 9.6 | 13.8 | 32.8 | 17.9 | 26.3 | 19.0 | 9.4 | 14.3 | 18.6 | 9.1 | 14.0 | 32.5 | 21.1 | 27.7 |
| Wafanyakazi waliojiajiri na wafanyakazi wao | 4.0 | 1.7 | 2.8 | 3.9 | 1.7 | 2.8 | 7.9 | 1.2 | 5.0 | 2.3 | 1.2 | 1.8 | 2.2 | 1.1 | 1.7 | 6.4 | 2.4 | 4.7 |
| Wafanyakazi waliojiajiri bila wafanyakazi | 56.6 | 37.8 | 47.4 | 56.7 | 37.1 | 47.0 | 53.4 | 69.2 | 60.3 | 59.7 | 48.6 | 54.3 | 59.8 | 48.2 | 54.2 | 55.4 | 64.7 | 59.3 |
| Wanachama wa ushirika wa uzalishaji mali | – | – | – | – | – | – | – | – | – | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 1.0 | 0.6 | 0.8 |
| Wasaidizi kazi za kaya bila malipo | 21.0 | 50.7 | 35.6 | 21.5 | 51.6 | 36.3 | 5.8 | 11.7 | 8.4 | 18.1 | 40.4 | 29.0 | 18.6 | 41.1 | 29.5 | 4.3 | 10.6 | 6.9 |
| Waajiriwa wengine | – | – | – | – | – | – | – | – | – | 0.6 | 0.5 | 0.5 | 0.6 | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.5 |
| **JML** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |







Hakimiliki © 2021 – NBS na OCGS

**Jedwali Na. 2.2: Asilimia ya Watu Walioajiriwa kwa Hali za Ajira, Wenye Miaka 15+ (Tafsiri ya Kimataifa)**

| Hali ya Ajira | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Wafanyakazi wanaolipwa | 17.8 | 9.5 | 13.7 | 17.4 | 9.3 | 13.4 | 32.9 | 17.7 | 26.2 | 18.6 | 9.0 | 13.9 | 18.2 | 8.8 | 13.5 | 32.5 | 21.1 | 27.7 |
| Wafanyakazi waliojiajiri na wafanyakazi wao | 3.8 | 1.6 | 2.7 | 3.7 | 1.6 | 2.7 | 8.1 | 1.3 | 5.1 | 2.3 | 1.1 | 1.7 | 2.2 | 1.1 | 1.6 | 6.4 | 2.4 | 4.7 |
| Wafanyakazi waliojiajiri bila wafanyakazi | 57.8 | 39.4 | 48.7 | 57.9 | 38.8 | 48.4 | 53.3 | 69.4 | 60.4 | 58.3 | 46.7 | 52.6 | 58.4 | 46.3 | 52.5 | 55.4 | 64.7 | 59.3 |
| Waajiriwa katika vyama vya ushirika | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 1.0 | 0.6 | 0.8 |
| Wasaidizi kazi za kaya bila malipo | 20.6 | 49.5 | 34.8 | 21.1 | 50.3 | 35.5 | 5.8 | 11.6 | 8.3 | 20.0 | 42.7 | 31.1 | 20.5 | 43.4 | 31.7 | 4.4 | 10.7 | 7.0 |
| Waajiriwa wengine | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.6 | 0.4 | 0.5 | 0.6 | 0.4 | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.5 |
| **JML** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Ujumbe muhimu: Jedwali 2.1** linaonesha kiwango kidogo cha ongezeko la watu walio kwenye ajira za malipo kutoka asilimia 14.1 hadi 14.3. Hiki ni kiashiria kizuri kinachopima ongezeko la ajira zenye hadhi. Hata hivyo waliojiari wenyewe bila ya wafanyakazi kwa kutumia tafsiri ya Kitaifa imeongezeka kutoka asilimia 47.4 mwaka 2014 kufikia 54.3 mwaka 2020/21. Vilevile, kiwango cha wasaidizi katika kazi za kaya bila malipo, mfano uuzaji wa duka la kaya bila malipo kimepungua kutoka asilimia 34.8 mwaka 2014 hadi asilimia 31.1 mwaka 2020/21.

**Mahusiano ya kisera:** Kiwango kidogo cha ongezeko la ajira yenye malipo katika kipindi cha miaka mitano (2014- 2020/2021) kunaweza kutafsiriwa kwamba, uchumi haukuweza kuzalisha kazi zenye hadhi ya kulipwa ujira. Hii inatoa ujumbe muhimu wa kisera kuhusu kuweka na kutekeleza sera madhubuti zinazovutia uwekezaji kwenye maeneo yanayotoa ajira nyingi na kwa kuzingatia umuhimu wa sekta binafsi kama kitovu cha kusukuma ukuaji wa uchumi na kuzalisha ajira, kuna umuhimu wa kuweka vivutio mahususi kwa sekta binafsi inayoonesha kuzalisha ajira nyingi na zenye hadhi ya kulipwa ujira stahiki.

Pamoja na ongezeko la watu wali kwenye ajira za malipo, kuna ongezeko la watu wanaojiajiri wenyewe, ambao wengi wanatokana na kaya zinzojihusisha na kilimo cha kujikimu. Kutokana na hali hiyo, sera zinazolenga kuongeza mazao thamani na kukifanya kilimo kuwa cha kibiashara ni muhimu kuongeza kipato cha wakulima wadogo na kuoingeza tija katika uzalishaji. Uwepo wa sera hizo utasaidia kubadili hali nzima ya ajira, kuongezeka kwa ajira na kupanuka kwa wigo wa kodi. Kwa upande mwingine, kuna sababu yay a kuendelea na utekelezaji wa sera zinazolenge maendeleo ya sekta zinazoibuka ikiwemo Sanaa na utamaduni, michezo na burudani. Katika miaka ya karibuni, sekta hizi zimethibitisha uwezo wake wa kuzalisha ajira nyingi hususa kwa vijana na kusaidia ongezeko la shughuli za kiuchumi.

Hakimiliki © 2021 – NBS na OCGS

# 3.0 AJIRA KWA SEKTA (EMPLOYMENT BY SECTOR)

Kiashiria cha Ajira kwa sekta kimegawanyika katika makundi makubwa yanayohusu shughuli za kiuchumi. Kiashiria hiki kinaonesha mgawanyiko wa ajira kisekta.

**Jedwali Na. 3.1: Asilimia ya Watu Walioajiriwa kwa Sekta, Wenye Miaka 15+ (Tafsiri ya Kitaifa)**

| Sekta | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Serikali Kuu na Serikali za Mitaa | 3.9 | 2.8 | 3.3 | 3.6 | 2.6 | 3.1 | 13.9 | 9.5 | 12.0 | 3.0 | 2.1 | 2.6 | 2.8 | 1.9 | 2.4 | 10.5 | 11.1 | 10.7 |
| Taasisi za umma | 0.5 | 0.1 | 0.3 | 0.6 | 0.1 | 0.3 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.5 | 0.2 | 0.3 | 0.5 | 0.2 | 0.3 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| Vyama vya siasa, NGO's, Mashirika ya dini | 0.7 | 0.4 | 0.5 | 0.7 | 0.4 | 0.5 | 0.4 | 0.3 | 0.3 | 2.5 | 1.2 | 1.9 | 2.6 | 1.2 | 1.9 | 1.3 | 0.9 | 1.1 |
| Mashirika ya Kimataifa au Mabalozi wa nje | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | - | - | - |
| Shughuli binafsi (Isiyo kilimo) | 29.4 | 23.8 | 26.6 | 28.9 | 23.3 | 26.1 | 47.5 | 45.2 | 46.5 | 24.1 | 21.1 | 22.7 | 23.4 | 20.6 | 22.0 | 48.5 | 47.3 | 48.0 |
| Ushirika uliosajiliwa au Vyama vya ushirika | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.4 | 0.1 | 0.3 | 1.6 | 0.5 | 1.1 | 1.6 | 0.5 | 1.0 | 2.9 | 1.6 | 2.4 |
| Shamba la binafsi au la familia au la kaya | 63.8 | 70.0 | 66.8 | 64.5 | 70.5 | 67.5 | 37.1 | 43.3 | 39.8 | 56.6 | 60.3 | 58.4 | 57.4 | 60.9 | 59.1 | 30.3 | 29.5 | 29.9 |
| Wafanyakazi wasiolipwa-Kaya | 0.1 | 0.2 | 0.2 | 0.1 | 0.2 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 3.8 | 7.2 | 5.5 | 3.9 | 7.3 | 5.6 | 1.0 | 3.4 | 2.0 |
| Shughuli nyingine za kaya za kiuchumi | 1.5 | 2.7 | 2.1 | 1.5 | 2.8 | 2.1 | 0.9 | 1.5 | 1.2 | 7.7 | 7.4 | 7.6 | 7.8 | 7.4 | 7.6 | 5.5 | 6.2 | 5.8 |
| **Jumla** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |





Hakimiliki © 2021 – NBS na OCGS

**Jedwali Na. 3.2: Asilimia ya Watu Walioajiriwa kwa Sekta, Wenye Miaka 15+ (Tafsiri ya Kimataifa)**

| Sekta | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Serikali kuu na Serikali za Mitaa | 3.7 | 2.7 | 3.2 | 3.5 | 2.5 | 3.0 | 13.5 | 9.3 | 11.6 | 2.9 | 2.1 | 2.5 | 2.7 | 1.9 | 2.3 | 10.5 | 11.1 | 10.7 |
| Taasisi za umma | 0.5 | 0.1 | 0.3 | 0.6 | 0.1 | 0.3 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.5 | 0.2 | 0.3 | 0.5 | 0.2 | 0.3 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| Vyama vya siasa, NGO's, Mashirika ya dini | 0.7 | 0.4 | 0.5 | 0.7 | 0.4 | 0.5 | 0.4 | 0.3 | 0.3 | 2.5 | 1.2 | 1.8 | 2.5 | 1.2 | 1.8 | 1.3 | 0.9 | 1.1 |
| Mashirika ya Kimataifa au Mabalozi wa nje | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | - | - | - |
| Shughuli binafsi (Isiyo kilimo) | 29.4 | 23.8 | 26.6 | 28.9 | 23.3 | 26.1 | 47.5 | 45.2 | 46.5 | 23.6 | 20.4 | 22.0 | 22.9 | 19.8 | 21.4 | 48.4 | 47.3 | 48.0 |
| Mashirika yaliyosajiliwa au Vyama vya ushirika | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.4 | 0.1 | 0.3 | 1.6 | 0.5 | 1.0 | 1.5 | 0.5 | 1.0 | 2.9 | 1.6 | 2.4 |
| Shamba la binafsi au la familia(/kaya) | 63.8 | 70.0 | 66.8 | 64.5 | 70.5 | 67.5 | 37.1 | 43.3 | 39.8 | 57.2 | 61.1 | 59.1 | 57.9 | 61.8 | 59.8 | 30.2 | 29.5 | 29.9 |
| Wafanyakazi wasiolipwa-Kaya | 0.1 | 0.2 | 0.2 | 0.1 | 0.2 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 4.0 | 7.4 | 5.7 | 4.1 | 7.5 | 5.8 | 1.0 | 3.5 | 2.0 |
| Shughuli nyingine za kaya za kiuchumi | 1.5 | 2.7 | 2.1 | 1.5 | 2.8 | 2.1 | 0.9 | 1.5 | 1.2 | 7.7 | 7.3 | 7.5 | 7.7 | 7.3 | 7.5 | 5.5 | 6.3 | 5.8 |
| **Jumla** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Ujumbe muhimu: Jedwali Na. 3.1** linaonesha kuwa hakuna mabadiliko makubwa ya mgawanyo wa ajira kisekta kwa kutumia tafsiri ya Kitaifa kati ya mwaka 2014 na 2020/21 japokuwa ajira katika Serikali Ku una Serikali za Mitaa zilisinyaa. Mabadiliko makubwa ya mgawanyo wa ajira yameonekena miongoni mwa watu walioajiriwa katika sekta ya kilimo (66.8% 2014 na 58.4% 2020/2021) na shughuli nyingine binafsi za kiuchumi zisizo za kilimo (mwaka 2014 asilimia 26.6, na mwaka 2020/21 asilimia 22.7).

**Mahusiano ya Kisera:** Kusinyaa kwa kiwango cha waajiriwa Serikalini kunatoa taswira kamili yah atua zilizochukuliwa na Serikali kati yam waka 2015 na 2020 ambapo zilitolewa ajira mpya chache. Pamoja na hatua hizi kusaidia kupunguza kukua kwa kiwango cha mishahra ya Serikali, kunaweza kuathiri utekelezaji wa sera kama zilivyopangwa kutekelezwa katika mikakati na mipango ya Serikali. Vilevile, inaweza kuathiri utekelezaji wa mikakati ya kurithishana madaraka ndani ya Serikali. Kupungua kwa kiwango cha ajira katika sekta binafsi za kiuchumi zisizo za kilimo kunaashiria uwekezaji mdogo katika sekta hizo ama uwekezaji umejikita katika maeneo yanayohitaji nguvu kazi kidogo. Halii inatoa ujumbe kwamba zinahitajika juhudi kubwa kuvutia pia uwekezaji na biashara zenye uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira.

# 4.0 AJIRA KWA AINA YA KAZI (EMPLOYMENT BY OCCUPATION)

Kiashiria cha Ajira kwa aina ya kazi kinaelezea mgawanyo wa kazi kulingana na makundi makubwa ya aina za kazi kama ilivyoainishwa kwenye Kamusi ya kazi ya Tanzania (TASCO). Mabadiliko ya mgawanyo wa kazi kwa makundi ya kazi yanaweza kutumika katika kuchambua hatua za maendeleo ya uchumi kwenye nchi.

**Jedwali Na. 4.1: Asilimia ya Watu Walioajiriwa kwa Aina za Kazi, Wenye Miaka 15+ (Tafsiri ya Kitaifa)**

| Aina ya Kazi | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Wabunge, watawala na mameneja | 0.7 | 0.2 | 0.5 | 0.7 | 0.2 | 0.5 | 0.7 | 0.2 | 0.5 | 0.5 | 0.2 | 0.4 | 0.5 | 0.2 | 0.4 | 0.5 | 0.2 | 0.4 |
| Wataalamu | 1.4 | 0.4 | 0.9 | 1.3 | 0.4 | 0.9 | 2.0 | 1.1 | 1.6 | 1.1 | 0.5 | 0.8 | 1.0 | 0.5 | 0.8 | 2.6 | 2.7 | 2.6 |
| Mafundi na wataalamu wasaidizi | 2.2 | 2.3 | 2.3 | 2.1 | 2.3 | 2.2 | 5.1 | 6.4 | 5.7 | 0.8 | 0.6 | 0.7 | 0.7 | 0.4 | 0.6 | 4.8 | 7.5 | 6.0 |
| Makarani | 0.5 | 0.9 | 0.7 | 0.5 | 0.9 | 0.7 | 1.7 | 2.0 | 1.8 | 0.6 | 0.5 | 0.6 | 0.6 | 0.5 | 0.6 | 1.1 | 1.8 | 1.4 |
| Wafanyakazi wa huduma na wauza maduka | 9.7 | 10.2 | 9.9 | 9.5 | 10.1 | 9.8 | 18.6 | 11.0 | 15.2 | 9.4 | 18.5 | 13.8 | 9.2 | 18.4 | 13.7 | 17.2 | 23.2 | 19.7 |
| Wafanyakazi wa kilimo na uvuvi | 62.5 | 68.8 | 65.6 | 63.2 | 69.4 | 66.3 | 38.5 | 44.6 | 41.2 | 58.1 | 57.9 | 58.0 | 59.1 | 58.7 | 58.9 | 23.1 | 21.8 | 22.6 |
| Wafanyakazi wanaofanya kazi za mikono | 9.6 | 3.0 | 6.4 | 9.4 | 2.8 | 6.1 | 15.3 | 14.7 | 15.0 | 10.7 | 5.7 | 8.3 | 10.5 | 5.5 | 8.0 | 16.5 | 16.8 | 16.6 |
| Waendeshaji wa mashine na waunganishaji wa mitambo | 5.2 | 0.2 | 2.7 | 5.2 | 0.2 | 2.7 | 6.2 | 0.4 | 3.7 | 4.5 | 0.6 | 2.6 | 4.5 | 0.6 | 2.6 | 3.3 | 0.0 | 1.9 |
| Kazi za kawaida zisizohitaji ujuzi (Elementary Occupations) | 8.2 | 13.9 | 11.0 | 8.1 | 13.7 | 10.9 | 11.8 | 19.5 | 15.2 | 14.4 | 15.4 | 14.9 | 13.9 | 15.1 | 14.5 | 30.8 | 26.0 | 28.8 |
| **JML** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |



**Jedwali Na. 4.2: Asilimia ya Watu Walioajiriwa kwa Aina ya Kazi,Wenye Miaka 15+ (Tafsiri ya Kimataifa)**

| Aina ya Kazi | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Wabunge, watawala na mameneja | 0.7 | 0.2 | 0.5 | 0.7 | 0.2 | 0.5 | 0.7 | 0.2 | 0.5 | 0.5 | 0.2 | 0.4 | 0.5 | 0.2 | 0.4 | 0.5 | 0.2 | 0.4 |
| Wataalamu | 1.3 | 0.4 | 0.9 | 1.3 | 0.4 | 0.8 | 2.0 | 1.1 | 1.6 | 1.1 | 0.5 | 0.8 | 1.0 | 0.5 | 0.8 | 2.6 | 2.7 | 2.6 |
| Mafundi na wataalamu wasaidizi | 2.1 | 2.2 | 2.2 | 2.0 | 2.1 | 2.1 | 5.0 | 6.2 | 5.5 | 0.8 | 0.6 | 0.7 | 0.7 | 0.4 | 0.5 | 4.8 | 7.5 | 5.9 |
| Makarani | 0.5 | 0.8 | 0.7 | 0.5 | 0.8 | 0.6 | 1.6 | 1.9 | 1.8 | 0.6 | 0.5 | 0.6 | 0.6 | 0.5 | 0.5 | 1.1 | 1.8 | 1.4 |
| Wafanyakazi wa huduma na maduka | 9.3 | 9.9 | 9.6 | 9.1 | 9.8 | 9.5 | 18.4 | 11.2 | 15.3 | 9.4 | 18.2 | 13.7 | 9.1 | 18.0 | 13.5 | 17.2 | 23.2 | 19.7 |
| Wafanyakazi wa kilimo na uvuvi | 63.9 | 69.8 | 66.8 | 64.6 | 70.3 | 67.4 | 38.3 | 44.3 | 40.9 | 58.6 | 58.8 | 58.7 | 59.6 | 59.6 | 59.6 | 23.1 | 21.8 | 22.6 |
| Wafanyakazi wanaofanya kazi za mikono | 9.3 | 2.9 | 6.1 | 9.1 | 2.6 | 5.9 | 15.5 | 14.9 | 15.3 | 10.4 | 5.5 | 8.0 | 10.3 | 5.3 | 7.8 | 16.6 | 16.8 | 16.7 |
| Wafanyakazi wanaoendesha na kuunganisha mitambo | 5.0 | 0.2 | 2.6 | 4.9 | 0.2 | 2.6 | 6.2 | 0.4 | 3.6 | 4.4 | 0.6 | 2.5 | 4.4 | 0.6 | 2.5 | 3.3 | 0.0 | 1.9 |
| Kazi za kawaida zisizohitaji ujuzi (Elementary Occupations) | 7.9 | 13.5 | 10.7 | 7.8 | 13.4 | 10.6 | 12.3 | 19.6 | 15.5 | 14.3 | 15.1 | 14.7 | 13.8 | 14.9 | 14.3 | 30.8 | 26.0 | 28.8 |
| **Jumla** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Ujumbe muhimu:** Jedwali namba 4.1 linaonesha mwenendo unaofanana baina ya aina za kazi mbalimbali kati ya mwaka 2014 na 2020/2021. Hata hivyo, makundi mawili yanahitaji kuangaliwa kiundani ili kutoa tafsiri na maeneo ya kisera yayohitaji kupatiwa ufumbuzi. Eneo la kwanza ni kupungua kwa ajira miongoni mwa mafundi pamoja na kazi nyingine zinazofanana nazo kutoka asilimia 2.2 mwaka 2014 hadi asilimia 0.7 mwaka 2020/2021; na kupungua kwa ajira kwa wataalam katika sekta ya kilimo na uvuvi kutoka 66.8% hadi 58.7. Kupungua ajira kwa kada ya mafundi kunaashiria kwamba, kada hii muhimu hususan kwenye sekta ya viwanda haiajiriki. Kuhusu wataalam wa kilimo na uvuvi inaashiria kwamba sekta hizi muhimu zinaweza kukumbwa na uhaba wa utaalam na hivyo kuathiri tija.

**Mahusiano ya kisera:**

- Kwa nchi kama Tanzania ambayo inafanya mageuzi ya kiuchumi kwa kujielekeza kwenye mapinduzi ya viwanda huku ikijielekeza kuimarisha mafunzo ya ufundi ili kuzaisha nguvu kazi yenye utaalam, hatua za kufungamanisha sera ya Elimu na Mafunzo na mapinduzi ya viwanda ni muhimu. Mafunzo yanabidi kulenga kuzalisha nguvu kazi inayohitajika katika soko la ajira na siyo kutoa mafunzo ambayo yatachukulia kwamba ndivyo soko la ajira linavyotaka. Kutokana na hilo, ni muhimu kuwepo na mpango wa muda mrefu wa kuendeleza rasilimali watu kwa ajili ya uchumi ili vyuo vya elimu ya mafunzo ya ufundi na vya elimu ya juu vizalishe nguvu kazi yenye ujuzi unaotakiwa na soko la ajira.
- Kupungua kwa nguvu kazi katika sekta ya kilimo ni ishara ya mapinduzi katika sekta hiyo. Hata hivyo, kupungua kwa nguvu kazi yenye utaalam kwenye sekta hii muhimu kunaweza kuwa na athari kubwa kwenye tija. Hivyo, sera zinazolenga kuvutia, kubakisha na kuajiri wataalam wa kilimo pale wengine wanapostaafu ni muhimu ili wataalam hao wawasaidie wakulima kwenye utoaji wa huduma za ugani na hivyo kuongezeka tija kwenye kilimo, mifugo na uvuvi.

# 5.0 USHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA WATU WENYE ULEMAVU (PARTICIPATION OF DISABLED PERSONS IN ECONOMIC ACTIVITIES)

Sehemu hii inaonesha ushiriki wa watu wenye ulemavu katika shughuli za kiuchumi, viashiria katika sehemu hii vimewasilishwa kama sehemu ya watu wenye ulemavu pekee.

**Jedwali 5.1: Ushiriki Katika Shughuli za Kiuchumi kwa Watu Wenye Ulemavu kwa Eneo na Jinsi, Wenye Miaka 15+ (Tafsiri ya Kitaifa)**

| Hali kuhusiana na Nguvu Kazi | 2014 | | | | | | | | | 2020-2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Wenye Ajira | 64.6 | 55.3 | 59.1 | 64.7 | 55.5 | 59.3 | 57.4 | 47.0 | 51.8 | 67.6 | 60.1 | 63.2 | 68.0 | 60.4 | 63.5 | 48.1 | 39.7 | 43.4 |
| Ukosefu wa Ajira | 9.5 | 14.6 | 12.4 | 9.5 | 14.6 | 12.4 | 8.4 | 14.9 | 11.7 | 4.4 | 7.2 | 6.0 | 4.3 | 7.0 | 5.8 | 16.0 | 21.7 | 19.1 |
| Nje ya Nguvukazi | 28.6 | 35.2 | 32.5 | 28.4 | 35.0 | 32.3 | 37.4 | 44.8 | 41.4 | 29.2 | 35.3 | 32.8 | 29.0 | 35.1 | 32.5 | 42.8 | 49.2 | 46.4 |

**Jedwali 5.2: Ushiriki Katika Shughuli za Kiuchumi kwa Watu Wenye Ulemavu kwa Eneo na Jinsi, Wenye Miaka 15+ (Tafsiri ya Kimataifa)**

| Hali kuhusiana na Nguvu Kazi | 2014 | | | | | | | | | 2020-2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Wenye Ajira | 70.8 | 61.5 | 65.3 | 71.0 | 61.8 | 65.6 | 58.9 | 49.2 | 53.7 | 68.3 | 61.4 | 64.2 | 68.7 | 61.7 | 64.6 | 48.1 | 39.7 | 43.4 |
| Ukosefu wa Ajira | 0.9 | 5.1 | 3.2 | 0.8 | 5.0 | 3.1 | 5.9 | 10.9 | 8.4 | 3.5 | 5.1 | 4.4 | 3.3 | 4.9 | 4.2 | 16.0 | 21.7 | 19.1 |
| Nje ya Nguvukazi | 28.6 | 35.2 | 32.5 | 28.4 | 35.0 | 32.3 | 37.4 | 44.8 | 41.4 | 29.2 | 35.3 | 32.8 | 29.0 | 35.1 | 32.5 | 42.8 | 49.2 | 46.4 |

**Ujumbe Muhimu: Matokeo katika Jedwali 5.1** yanaonesha kuwa ajira baina ya watu wenye ulemavu kwa kutumia tafsiri ya Kitaifa imeongezeka kutoka asilimia 59.1 mwaka 2014 hadi asilimia 63.2 mwaka 2020/21. Aidha takwimu zinaonesha pia kuwa, ukosefu wa ajira kati ya watu wenye ulemavu umepungua sana kutoka asimilia 12.4 mwaka 2014 hadi asilimia 6.0 mwaka 2020/21.

**Mahusiano ya kisera:** Ongezeko la ajira baina ya watu wenye ulemavu linaonesha mafanikio ya utekelezaji wa Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004 inayosisitiza ukuzaji wa ajira kwa watu wenye ulemavu. Aidha, kuanzishwa kwa dirisha maalumu la mikopo kwa watu wenye ulemavu (asilimia 2 ya mapato ya ndani ya halmashauri) kumechangia ukuzaji wa ajira kwa watu wenye ulemavu. Ili kuwepo na uendelevu wa hali hii nzuri, kunahitajika juhudi kubwa katika kuingiza masuala ya walemavu kwenye sera nyingine ili watu wenye ulemavu wasiachwe nyuma. Hatua hizi ni lazima ziendane na zoezi la kuwabainisha na kuwasijili watu wenye ulemavu katika jamii.

# 6.0 KIWANGO CHA USHIRIKI KATIKA NGUVU KAZI (LABOUR FORCE PARTICIPATION RATE)

Kiwango cha ushiriki wa Nguvu Kazi ni uwiano wa watu wanaofanya kazi pamoja na wasiokuwa na ajira wakilinganishwa na watu wenye umri wa kufanya kazi nchini. Kiashiria hiki kinapima mwenendo wa nguvu kazi inayoweza kushiriki kwenye uzalishaji wa bidhaa na huduma.

**Jedwali Na. 6.1: Viwango vya Ushiriki Katika Nguvu Kazi, Wenye Miaka 15+**

| Eneo | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Vijijini | 91.9 | 87.5 | 89.7 | 92.1 | 87.7 | 89.8 | 87.2 | 80.3 | 83.7 | 88.0 | 82.0 | 84.9 | 88.2 | 82.2 | 85.1 | 83.5 | 71.0 | 77.1 |
| Miji mingine | 86.4 | 81.7 | 83.9 | 86.8 | 82.3 | 84.4 | 78.9 | 70.0 | 74.3 | 82.9 | 77.6 | 80.0 | 83.2 | 78.2 | 80.4 | 79.6 | 70.3 | 74.8 |
| DSM | 81.3 | 71.5 | 76.2 | 81.3 | 71.5 | 76.2 | - | - | - | 78.8 | 74.3 | 76.4 | 78.8 | 74.3 | 76.4 | - | - | - |
| **JML** | **89.2** | **84.0** | **86.5** | **89.4** | **84.2** | **86.7** | **83.4** | **75.6** | **79.4** | **86.1** | **80.3** | **83.1** | **86.3** | **80.6** | **83.3** | **81.6** | **70.7** | **76.0** |

Kiwango cha ushiriki katika nguvu kazi kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) kimepungua kutoka 86.5% mwaka 2014 hadi 83.1% mwaka 2020/21 (Jedwali 6.1).

**Ujumbe muhimu:** Kupungua kwa kiwango cha ushiriki katika Nguvu kazi kumechangiwa kwa sehemu kubwa na juhudi chanya za uaandaji wa nguvu kazi bora miaka ya baadae kutokana na kuongezeka kwa udahili mashuleni kufuatia utoaji wa elimu bila malipo na kuongezeka kwa wanufaika na mikopo ya elimu ya juu na hivyo kuwatoa watu kwenye kundi la nguvu kazi.



# 7.0 UWIANO WA AJIRA KWA IDADI YA WATU WENYE UMRI WA MIAKA 15 + (EMPLOYMENT TO POPULATION RATIO)

Kiashiria cha Uwiano wa ajira kwa Idadi ya Watu wenye umri wa kufanya kazi hupima kiwango cha watu wanaofanya kazi ikilinganishwa na watu wote wenye umri wa kufanya kazi. Mtu anahesabika kuwa anafanya kazi ikiwa katika kipindi maalum cha rejea (wiki iliyopita) alikuwa anafanya kazi kwa malipo, amejiajiri mwenyewe (na wafanyakazi au bila wafanyakazi), Wanaushirika, na Wanaofanya Kazi za kusaidia katika Familia, au Wafanyakazi wengine wanaojifunza kazi (Wanagenzi, Walio kwenye mafunzo ya Vitendo mahali pa kazi nk.).

**Jedwali Na. 7.1: Uwiano wa Ajira kwa Idadi ya Watu Wenye Umri wa Miaka 15+ (Tafsiri ya Kitaifa)**

| Eneo | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Vijijini | 84.6 | 79.6 | 82.1 | 84.7 | 79.9 | 82.2 | 82.2 | 68.1 | 75.0 | 83.5 | 74.1 | 78.7 | 83.6 | 74.6 | 79.0 | 78.6 | 54.9 | 66.5 |
| Mijini Mingine | 79.9 | 70.6 | 74.9 | 80.5 | 72.0 | 76.0 | 67.8 | 41.8 | 54.4 | 78.4 | 65.2 | 71.2 | 79.4 | 66.8 | 72.5 | 67.2 | 44.3 | 55.3 |
| DSM | 72.1 | 48.5 | 59.8 | 72.1 | 48.5 | 59.8 | - | - | - | 69.5 | 53.1 | 60.8 | 69.5 | 53.1 | 60.8 | - | - | - |
| **JML** | **81.9** | **73.3** | **77.4** | **82.1** | **73.8** | **77.8** | **75.6** | **56.0** | **65.5** | **81.1** | **70.1** | **75.4** | **81.4** | **70.7** | **75.8** | **73.1** | **49.7** | **61.0** |

**Jedwali Na. 7.2: Uwiano wa Ajira kwa Idadi ya Watu Wenye Umri wa Miaka 15+ (Tafsiri ya Kimataifa)**

| Eneo | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Vijijini | 90.3 | 84.7 | 87.4 | 90.5 | 85.0 | 87.7 | 84.6 | 70.6 | 77.4 | 86.1 | 78.1 | 81.9 | 86.2 | 78.6 | 82.3 | 78.6 | 54.9 | 66.5 |
| Mijini Mingine | 83.4 | 74.0 | 78.4 | 84.1 | 75.6 | 79.5 | 71.0 | 43.9 | 57.0 | 78.8 | 65.6 | 71.6 | 79.8 | 67.2 | 72.9 | 67.3 | 44.3 | 55.4 |
| DSM | 73.4 | 49.2 | 60.8 | 73.4 | 49.2 | 60.8 | - | - | - | 69.5 | 53.1 | 60.8 | 69.5 | 53.1 | 60.8 | - | - | - |
| **JML** | **86.5** | **77.4** | **81.8** | **86.7** | **78.0** | **82.2** | **78.4** | **58.3** | **68.0** | **83.0** | **72.9** | **77.7** | **83.3** | **73.6** | **78.2** | **73.2** | **49.7** | **61.1** |

Hakimiliki © 2021 – NBS na OCGS

**Ujumbe muhimu: Jedwali 7.1** linaonesha kuwa, kwa tafsiri ya Kitaifa kiwango cha uwiano cha wenye ajira kwa idadi ya watu wenye umri wa miaka 15+ kwa JMT kimepungua kutoka 77.4% mwaka 2014 hadi 75.4% mwaka 2020/21. Kupungua huko kumechangiwa na idadi kubwa ya nguvukazi kudahiliwa katika ngazi mbali mbali za elimu kutokana na juhudi za Serikali za kutoa elimu bila malipo na kuongeza wigo wa wanufaika wa elimu ya juu ikilinganishwa na uwezo wa kuzalisha ajira kitaifa.

**Mahusiano ya Kisera katika ushiriki wa Nguvukazi na Uwiano katika Ajira:**

- Juhudi za Serikali kutoa elimumsingi bila malipo imechangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa kiwango cha uwiano wa ajira kwa idadi ya watu. Juhudi hizi za Serikali zitawezesha upatikanaji wa wataalam wengi wenye ujuzi miaka ya mbele jambo ambalo wadau wanapaswa kuliunga mkono. Sababu nyingine zilizosababisha kupungua uwiano wa nguvu kazi ni pamoja ulemavu, magonjwa na kazi za msimu pamoja na kutegemea kilimo ambacho kinaathiriwa sana na misimu.
- Kadri ya uchumi wa Tanzania unavyokua, mipango ya muda mrefu na maoteo ya nguvu kazi ni muhimu kufanyika. Viwango vikubwa vya kuzaliana miongoni mwa watanzania, vinatoa angalizo la kupanua miundombinu ya elimu na wataalam katika ngazi zote pamoja na ukuaji wa uchumi unaoajiri watu wapya wanaoingia kwenye soko la ajira. Ongezeko kubwa la watu lisiloendana na ukuaji wa uchumi unaozalisha ajira utasababisha wastani wa uwiano katika ajira ikilinganishwa na idadi ya watu kuzidi kupungua.

.



# 8.0 SAA ZA KAZI (HOURS OF WORK)

Saa za Kazi ni kipimo cha wastani wa muda ambao watu hutumia kwenye shughuli za uzalishaji wa bidhaa na huduma. Uchambuzi wa muda wa kazi umefanyika kwa kuangalia Saa za Kazi za Kawaida (Usual Hours of Work) na Saa za Kazi za Sasa (Current Hours of Work).

## 8.1 Saa za Kazi za Kawaida (Usual Hours of Work)

Saa za Kazi za Kawaida ni wastani wa muda ambao kwa kawaida watu hutumia kwenye shughuli za uzalishaji wa bidhaa na huduma kila siku.

**Jedwali Na. 8.1.1: Wastani wa Saa za Kazi za Kawaida kwa Wiki kwa Wenye Umri wa Miaka 15+ (Tafsiri ya Kitaifa)**

| Hali ya Ajira | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Wafanyakazi wanaolipwa | 65 | 59 | 63 | 66 | 59 | 63 | 60 | 48 | 56 | 65 | 58 | 63 | 65 | 59 | 63 | 61 | 46 | 57 |
| Wafanyakazi waliojiajiri na wafanyakazi wao | 71 | 64 | 69 | 71 | 64 | 69 | 65 | 51 | 63 | 70 | 66 | 69 | 70 | 67 | 69 | 67 | 52 | 64 |
| Wafanyakazi walijiajiri bila wafanyakazi | 60 | 52 | 57 | 60 | 52 | 57 | 58 | 42 | 50 | 59 | 49 | 55 | 59 | 50 | 55 | 57 | 41 | 50 |
| Waajiriwa katika vyama vya ushirika | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 58 | 48 | 56 | 58 | 52 | 56 | 60 | 31 | 51 |
| Wasaidizi kazi za kaya bila malipo | 45 | 45 | 45 | 45 | 45 | 45 | 30 | 31 | 31 | 47 | 43 | 44 | 47 | 43 | 44 | 35 | 32 | 33 |
| Waajiriwa wengine | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 56 | 46 | 52 | 55 | 47 | 52 | 61 | 37 | 51 |
| **JML** | **58** | **49** | **54** | **58** | **49** | **54** | **57** | **42** | **51** | **58** | **48** | **53** | **58** | **48** | **53** | **58** | **41** | **51** |

**Jedwali Na.8.1.2: Wastani wa Saa za Kazi za Kawaida Kwa Wiki kwa Wenye Umri wa Miaka 15+ (Tafsiri ya Kimataifa)**

| Hali ya Ajira | 2014 | | | | | | | | | 2020/2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | | JMT | | | TZB | | | ZNZ | | |
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| Wafanyakazi wanaolipwa | 65 | 59 | 63 | 66 | 60 | 64 | 60 | 48 | 56 | 65 | 58 | 63 | 65 | 59 | 63 | 61 | 46 | 57 |
| Wafanyakazi waliojiajiri na wafanyakazi | 70 | 64 | 69 | 71 | 64 | 69 | 65 | 49 | 63 | 70 | 66 | 69 | 70 | 67 | 69 | 67 | 52 | 64 |
| Wafanyakazi waliojiajiri bila wafanyakazi | 59 | 51 | 56 | **59** | 51 | 56 | 58 | 42 | 50 | 59 | 49 | 55 | 59 | 50 | 55 | 57 | 41 | 50 |
| Waajiriwa katika vyama vya ushirika | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 58 | 48 | 56 | 58 | 52 | 56 | 60 | 31 | 51 |
| Wasaidizi kazi za kaya bila malipo | 45 | 45 | 45 | 45 | 45 | 45 | 30 | 31 | 31 | 47 | 43 | 44 | 47 | 43 | 44 | 35 | 31 | 33 |
| Waajiriwa wengine | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 56 | 46 | 52 | 55 | 47 | 52 | 61 | 37 | 51 |
